

UTASHI WA KIUNGU NA MUHANGA WA HUSAIN (A.S.)

(Majlis ya ki-Urdu ya Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi (t.s.). Majlis iliyosomwa miaka ya 1980s.

Imefanyiwa tarjuma ya Kiingereza na Dr. Shabeeb Rizvi;

Imefanyiwa tarjuma ya Kiswahili kutoka ya Kiingereza na Dr. Muhammad Kanju;

Kimehaririwa na Sheikh Ali Jumaa Mayunga.)

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu
Baraka za Allah ziwe juu yako, Ewe Saaheb al-Amr, tusaidie na usituache*

Imam Husain (a.s.) alieleza:

شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَرَاني فَيَبْلُغَ

“Allah anataka kuniona mimi nauliwa kishahidi.”

Ilikuwa ni wakati Imam Husain (a.s.) alipokuwa anaaga kwenye kaburi la Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) na alikuwa analia sana. Akiwa katika hali hiyo ya majonzi makubwa usingizi ulimshika kwa muda mdogo na akaota kwamba Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) ametoka kaburini mwake mpaka kwenye kiono chake. Imam Husain (a.s.) alimkumbatia na kuguta: “Mpenzi babu! Tafadhali nichukue twende pamoja kaburini kwako.” Hapo ndipo Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akamtabiria:

شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَرَاكَ فَيَبْلُغَ...

“Ewe Husain! Unasafiri kwenda Iraq kwasababu Allah anataka kukuona wewe unauliwa kishahidi.”

Vilevile alimfahamisha kwamba aongozane na familia yake.

فِإِنَّ اللَّهَ شَاءَ أَنْ يَرَاهُنَّ سَبَأً

“Hakika Allah anapenda kuwaona wao wakiwa kama mateka.”

Nimewasilisha kwenu maelekezo haya ya Mjumbe wa Allah (s.a.w.w.) yote kwa pamoja. Inawezekana kabisa kwa mtu kufikiria kwamba hakika kitendo cha Yazid kilikuwa sahihi. Allah alipenda kumuona Imam Husain (a.s.) anauliwa shahidi na familia yake kuchukuliwa kama mateka. Bila shaka ametekeleza matakwa ya Allah. Kwa hiyo Yazid bila shaka ametenda kitendo kizuri na sahihi. Nimeyasoma maelezo haya mbele yenu kwa ajili tu ya kujibu aina hii ya upinzani ili kwamba niweze kuelezea kwa ufupi.¹

Ingawa naelewa kwamba muda unatukimbia lakini napenda nijibu kwa ufupi upinzani huu. Ilikuwa ni Utashi wa Allah (s.w.t.), kwamba Imam Husain (a.s.) auliwe kishahidi na familia yake tukufu ichukuliwe kama mateka. Hii ina maana gani haswa? Kama huu ulikuwa ni Utashi wa Allah, basi kifo cha kishahidi kilikuwa wajib juu ya Imam Husein (a.s.) na halikadhalika kuwekwa kizuizini kwa familia yake. Hakuna anayeweza kulipinga hili.

Lakini swali linalokuja ni iwapo ilikuwa ni wajib kwa Yazid (l.a) kumuua Imam Husain (a.s.) na kuwachukuwa mateka wanawake wake na watoto? Kama nikitumia istilahi za kidini, naweza kusema kwamba sharti la kujuzu kwa kitendo ni jaizi, lakini sharti la kuwepo sio (jaizi). Naweza kwa urahisi kuendelea kwa kulisema hili na hakuna atakayeweza kuelewa kile ambacho nimekisema punde tu. Hebu ngoja nielezee hili katika maneno rahisi kwamba kuna baadhi ya vitendo ambavyo ni wajibu juu ya kila mtu mzima na mwenye akili timamu na huhitajika kutekelezwa katika mazingira yote. Kwa mfano, swala na saumu ni wajibu katika mazingira yote kwa ye yeyote ambaye ni mtu mzima na asiye mwendawazimu. Kuna matendo machache ambayo huwa ni wajibu kwa utekelezaji tu wa masharti fulani. Kama masharti hayakukamilishwa, basi hayawi wajibu.

1 Mheshimiwa Baba yangu, Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi (Allah alibariki kaburi lake) alisoma Majlis hii kwa ajili ya kumbukumbu ya siku ya arobaini ya Mkuu wa Mashahidi Imam Husain (a.s.) wakati wa kipindi cha miaka ya katikati ya 1980 kijijiini kwetu Maloof, Gopalpur, Wilaya ya Siwan, Bihar, India. Imeandikwa kutoka kwenye mkanda wa sauti uliorikodi Majlis hiyo.

Kwa mfano, Hajj ina masharti machache kama vile siha, pesa na uwepo wa muda wa kutosha. Hebu tuchukulie kama mtu, pengine wewe, umeweza kupata pesa za kutosha kwa ajili ya kwenda Hijja tarehe 5 au 6 Dhul Hijja, lakini hutoweza kufika kule mapema. Kwa hiyo, inahitajika muda, siha, pesa, safari ya usalama na uhakika wa kuwa salama wakati wa kukaa huko angalau hisia ya msingi ya usalama, kwa vile hakuna awezaye kamwe kuwa na uhakika. Mbali na hili, pia lazima uwe na pesa za kutosha kiasi kwamba wakati wa kurudi huhitaji kuomba msaada kutoka kwa watu wengine. Muda wote ambao hutokuwepo nyumbani matumizi ya wanaokutegemea lazima yazingatiwe.

Ni wakati tu masharti haya yote yamekamilika, ndipo Hajj inapokuwa wajibu juu ya mtu, sio vinginevyo. Halikadhalika kwa Zakaat kama ana kiasi fulani cha mali na akabakia nayo kwa mwaka mzima, Zakaat itakuwa wajibu juu yake, sio kabla ya hili. Wakati masharti ya Jihadi yakikamilika hapo ndio tu itazingatiwa kuwa wajibu. Sio tu kutoka nyumbani mwako na upanga na kumshambulia kila mtu kwa upanga huo. Mtu kama huyu ataitwa mwendawazimu. Kwa hiyo, ina maana kwamba matendo fulani licha yakuwa wajibu kiuhalsia, yatakuwa wajibu kwangu au kwako kama tu masharti yake yamekamilika.

Sasa hebu ngoja nielezee tofauti kati ya matendo ya wajibat hizi mbili. Swala ni wajibu katika mazingira yote na hivyo ni muhimu kwetu kukamilisha masharti yake yote. Kwa mfano, kwa vile Wudhu huhitajika kabla ya swala, hilo pia litakuwa tendo la wajibu. Kama Tayyammum au Ghusl itakuwa mbadala wake, basi matendo haya yatakelezwa viliyvo kwa utaratibu wake. Kwa vile Swala ni kitendo cha wajibu ambacho hakina mahitaji yoyote, ni lazima itekelezwe kwa hali yoyote. Hivyo, vitendo vyote hivyo ambavyo kwavyo vinahitajia kuswihi kwake navyo vitatajwa kama wajibu, yaani, kupata maji halisi na safi, nguo za kutosheleza na sehemu safi kutockana na najisi kwa ajili ya kusujudia au kama ni lazima Tayammum ifanyike, basi upatikane udongo safi (usio na najisi) nk. Matendo yote haya yatakuwa wajibu juu yetu. Lakini kwa utekelezaji wa Hajj au Zakaat, kujuzu kwao ni kwa masharti na halikadhalika kwa Jihadi ni hivyo hivyo. Lakini kutekeleza masharti yao ya mwanzo sio wajibu wetu. Kama masharti hayo ya mwanzo yametekelezwa kama vile siha njema na gharama inayohitajika kwa ajili ya Hijja ipo, ndio hapo tu Hajj itakuwa wajibu. Lakini kama masharti ya mwanzo hayakukamilika, basi Hajj haitakuwa wajibu. Kwa namna yoyote haiwezi kusemwa kwamba kama siha inaturuhusu na masharti yote yapo tunayo (yamekamilika), isipokuwa pesa na matumizi ya safari, basi tunaweza kupora kwenye banki kwa sababu Hajj ni kitendo cha wajibu. Inaweza kuhitimishwa kwamba baadhi ya vitendo ni wajibu bila ya masharti na maandalizi yake kwa ajili ya mahitaji ya mwanzo pia ni wajibu kama sehemu ya utekelezaji wake wakati ambapo baadhi ya vitendo ni wajibu tu baada ya masharti yao ya mwanzo kukamilishwa. Sio wajibu juu yetu kutekeleza masharti hayo ya mwanzo.

Sasa hebu tuchambue iwapo matakwa ya Allah kwa ajili ya kifo cha kishahidi cha Husain (a.s.) kilikuwa kitendo kinachofanana na Swala na Saumu? Kama Shimr (l.a) asingemuwa, basi Imam (a.s.) angekata kichwa chake mwenyewe na kufa, kwa vile Allah alipenda kuona anauliwa kishahidi? Kwa hakika haikuwa wajibu kwa Imam Husein (a.s.) kwamba kama hakuna wa kumuua, basi angemlazimisha Hadhrat Abbas (a.s.) kumuua kwa vile Allah amependa kifo chake cha kishahidi. Kwa hakika haikuwa wajibu kwa familia ya Imam (a.s.) kuvua Hijab zao wenyewe na kujifunga pingu wenyewe kwa sababu tu Allah alipenda wawe katika hali hiyo. Kilichokuwa wajibu juu yao ilikuwa ni ukweli kwamba wakati Yazid aache wajibu wake, kisha basi wangekuwa tayari kukubali kifo cha kishahidi na kufungwa. Tunasikia kwamba Imam Husein (a.s.) alitahiniwa katika uwanda wa Karbala. Lakini tu Imam Husein (a.s.) hakua akijaribiwa. Hata Yazid, Ibn Ziyad, Umar Ibn Sa'ad (laana ya Allah iwe juu yao wote) wote walijaribiwa. Mtihani ulikuwa kwa kila mtu na yeoyote iwe ni Shimr, Khuli, Hurmala (laana ya Allah iwe juu yao wote) au yeoyote yule. Katika jeshi la asikari 32,000, hata yule aliyekuwa akiwalisha farasi chakula au maji alikwa akiwekwa kwenye mtihani wake. Kila mtu alikuwa akijaribiwa kwa wajibu ambao Allah ameamuru kwa ajili yao.

Sasa hebu tuangalie ni upi ulikuwa wajibu wa Yazid, Shimr na Umar Ibn Sa'ad (laana ya Allah iwe juu yao wote). Wewe na kila mtu angesema kwamba ilikuwa ni wajibu juu yao kula kiapo cha utii kwa Imam Husain (a.s.), kumkubali yeye kama kiongozi wao wa kweli, kufuata amri zake na kumchukulia yeye kama kiongozi na mwelekezaji wao. Yote hayo yalikuwa wajibu juu yao, lakini walishindwa kinyonge katika mtihani wao. Allah alimuumba kila mtu huru na mwenye kujitegemea kuchagua na kuoneshwa njia mbili kwa kila mtu ima kutembea katika njia iliyo sawa sawa na kupokea mwongozo au kufuata njia isiyo sahihi na kukengeuka kwenye moto wa Jahannamu.

إِنَّ هَذِهِ نَعْمَةُ اللَّهِ إِنَّمَا شَكِيرًا وَإِنَّمَا كَفُورًا

“Hakika tumemwongoza njia, ama awe ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.”²

Allah amefungua milango ya mwongozo kwa wote, hata kwa jeshi la Ibn Ziyad la asikari 32,000. Lakini kutokana na wale 32,000, ni 32 tu waliopokea mwongozo. Baada ya kusikiliza khutba za Imam Husain (a.s.) watu 32 kutoka jeshi la Yazid walijiunga na Imam Husain (a.s.). Mmoja katika elfu alipokea mwongozo wakati ambapo wale wengine (kwa hiari yao) walitembea kuelekea Jahannamu. Lau kama wote wangekubali mwongozo, yaani, lau wangefuzu katika mtihani wao, basi si kifo cha kishahidi kingekuwa wajibu kwa Imam Husain (a.s.) wala ufungwa kwa familia yake. Kwa vile walipewa uhuru na kuutumia vibaya uhuru huu, yaani, walichukua njia ya kimakosa (potofu), sasa ni upi wajibu juu ya Imam Husain (a.s.) na familia yake? Imam Husain (a.s.) hapa pia ana hiyari mbili. Kama wangekula kiapo cha utii kwa Imam Husain (a.s.) na kukubali uongozi wake, ingelikuwa ni wajibu kwa Imam Husain (a.s.) kuwaongoza. Lakini walipotoka na wakasisitiza kupigana na kuingia katika mapigano na Imam Husain (a.s.) na kumlazimisha kula kiapo cha utii kwa Yazid vinginevyo wangemkata kichwa. Kuanzia hapa na kuendelea, hata Imam Husein (a.s.) alikuwa na hiyari mbili. Hiyari moja ilikuwa ni kutumia tunu ya uwezo wake wa kiungu, kuliangamiza jeshi la Yazid na hatima yao kuwa wenye moto wa Jehannamu kwa ajili yao daima milele. Sisi wote tunafahamu ukweli huu; na ima tukiwa katika nusu usingizi, huzuni, ugonjwa au afya, kama mtu ye yeyote atauliza kuhusu hilo, jibu letu kwa dhahiri litakuwa kwamba lau Imam Husein (a.s.) angeelekeza tu, jeshi la Yazid lingeangamizwa

Imam Husain (a.s.) alikuwa bado ni kiongozi wa kiungu. Hata kama Janabe Zainab (s.a.) angelaani jeshi la Yazid, lingeangamia. Lau Janabe Zainab (s.a.) au Imam Husain (a.s.) angeelekeza, Mto Alqamah ungegeuka wenyewe na kuelekea kwenye mahema yao. Lakini sasa kwa vile jeshi la Yazid limechagua kosa na upotofu kwa ajili yao wenyewe na kuwa waasi, Allah alimuamuru Imam Husain (a.s.) kujizuiya kutumia uwezo wake wa kiungu wa Uimamu.

شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَرَاني فَتَبَارِكَ

“Allah alipenda kuniona mimi nikiuliwa shahidi na
baada ya kifo changu cha shahidi Alipenda kuionna familia yangu kama mateka”

Kutokana na mtazamo wa Imam Husain (a.s.), ingawa kifo cha kishahidi cha Ali Asghar (a.s.) na Ali Akbar (a.s.) ilikuwa ni misiba mikali lakini kuvuliwa Hijab kwa Zainab (s.a.) na Umm Kulthum (s.a.) ilikuwa ni maumivu makubwa. Ni kitu cha kutafakari kwamba Imam Husain (a.s.) katika maisha yake yote hajawahi kuwaona dada zake Zainab (s.a.) na Umm Kulthum (s.a.) bila ya Hijab. Bali, hata fikra ya tukio kama hilo lingesababisha machozi machoni mwake. Hebu fikiria hali ingekuaje kwa Imam Sajjad (a.s.) aliye kuwa mgonjwa mbele ya macho ya wale ambao Hijab ya Zainab (s.a.) na Umm Kulthum (s.a.) zilichukuliwa na chini ya uongozi wake, wanawake wale masharifu, waliondoka bila wenye kuwahifadhi na warithi, walifungwa kamba na kuburuzwa kwenye baraza la Yazid.

Hata hivyo, sababu kwa ajili ya uamuzi huu ni kwamba wakati Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alipomtabiria Imam Husain (a.s.) kwamba Allah anapenda kuona wewe unauliwa kishahidi na wanawake watukufu wa familia yako kama mateka, haina maana kwamba alichofanya Yazid kilikuwa ni kizuri. Bali, Yazid alishindwa kinyonge katika mtihani wake. Lakini baada ya kushindwa kwake, ikawa ni wajibu juu ya watu hawa kuvumilia majaribu na shida zilizowapata kwa subira na shukurani na kuacha uwezo wa kiungu na mamlaka ambayo Allah amewatunuku wao. Matokeo ya kutotumia uwezo wa kiungu ilikuwa ni kukataa msaada wa Majini na malaika. Ingawa hata hivyo aliomba msaada kutoka kwa watu,

هُلْ مِنْ نَاصِرٍ يَنْصُرُنَا

“Je, yuko ambaye atatusaidia?”

Hakuna popote ambapo walipenda kupigana vita nje ya uwezo wa kibinadamu.

² Surah Al-Insaan (76):3

Hata hivyo, sasa unaweza kuuliza ni kwanini Mtukufu Mtume (s.a.w.w) alisema kwamba ni utashi wa Allah kuona wanawake watukufu wa familia yako kama mateka. Tunaomba kinga kwa Allah! Haikuwa kwamba Allah ana uadui wowote na kwa wanawake wa familia ya Imam (a.s.). Tunaomba kinga kwa Allah! Hakika, ilikuwa kwa ajili ya uhai wa dini na viyi mchango huu kwenye uhai wa dini ulivyokuwa dhahiri katika matukio yote ya baadae. Lau kama matukio haya ya baadae yasingetukia, tungefikiria na kutafakari ni kwa nini msiba kama huu ulijitokeza kuwahuwa hawa watukufu. Hata hivyo, hakuna haja kwetu sisi kufikiria kuhusu hilo sasa kwa vile matukio yamehifadhiwa katika (vitabu vyta) historia kwa uwazi kabisa na tunaweza kwa urahisi kutoa hitimisho kutokana na matukio hayo.

Unaona baadhi ya watu wanasema kwamba Muawiyah (l.a) alikuwa mtu wa kwanza kuanzisha idara ya kwanza kabisa ya propaganda katika Syria. Alianzisha idara ya propaganda na wajumbe wake walikuwa masahaba wachache wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Taabi'ina wachache. Mionganoni mwa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambao walishiriki katika propaganda hii walikuwa ni Abu Hurairah, Mughira na Ibn Shuabah na mionganoni mwa Tabi'ina walikuwa ni Urwah bin Zubayr nk. Walikuwa wakilipwa pesa nyingi na jukumu lao lilikuwa ni kubuni na kughushi hadithi za kuwalaani na kuwatuhumu Ahlul Bayt wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kubuni hadithi za kumtukuza Muawiyah na Bani Umayyah (l.a).

Tukio lifuatalo litakupa mwelekeo wa viyi hali ilivyokuwa mbaya. Alikuwepo sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa jina akiitwa Samurah Ibn Jundab ambaye kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alimtabiria kwenda Jahannamu. Mtukufu Mtume aliwajulisha watu watatu kwamba atakayekufa wa mwisho mionganoni mwao atakwenda Jahannamu na Samurah Ibn Jundab alikufa mwisho. Siku moja Muawiyah (l.a) alimtaka aghushi hadithi. Aliuliza, “Ipi mojawapo?” Muawiyaha akajibu: “Kuhusiana na aya nne, tatu kati ya hizo zilikuwa kwa asili zikiwalaani wanafiki na ya nne ilikuwa ile iliyoteremshwa katika kumtukuza Ali (a.s.) wakati wa kuhamma.”

Muawiyah (l.a) akasema: “Uandike kwamba hizi aya tatu ni kwa ajili ya kumlaani Ali (a.s.) (Mungu aepushue mbali), ambapo ile ya nne: ‘Na mionganoni mwa watu yuko yule ambaye anauza . nafsi yake kwa kutaka radhi ya Allah³’ ni katika kumtukuza Ibn Muljam (l.a).” Samurah aliuliza kuhusu malipo ya kazi hiyo. Aliahidiwa dirham mia moja elfu. Akasema kwamba dirham mia moja elfu zilikuwa hazitoshii kwa hadith imara kama hiyo. Muawiya akaongeza mia mbili efu ambazo Samurah aliona pia hazitoshii. Muawiya akatoa mia tatu elfu lakini Samuraha akakataa. Wakati dirham mia nne elfu zipowekwa mbele yake, alikubali na akaandika: “Aya tatu ambazo zilikuwa katika kuwalaani wanafiki zinahusiana na Ali (a.s.) (Mungu aepushie mbali); zile ambazo husema: ‘Wameuza nafsi zao kwa radhi ya Allah’ zinamhusu Ibn Muljam.”

Sitaki nifafanue zaidi ya hapa lakini wazee wamesimulia kwamba Janab Sibte Hasan (Allah ainyanyue hadhi yake) alisoma siku moja katika Majlis kwamba Muawiyah (l.a) alikuwa na uwezo wa kughushi hadith lakini hakuweza kuficha ukweli kwamba ni ya kughushi.

Kwa kiasi kikubwa, Bani Umayyah waliweza kuwashawishi Wasyria kwamba Muawiyyah na Yazid walikuwa ndugu wa karibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na watoto na kijana walilelewa katika itikadi sawa. Lakini hadithi za kughushi kama hizo zilizotajwa hapo juu zilienezwa kuhusiana na Ali (a.s.) na Ahlul Bayt (a.s.).

Kiwango cha akili ya watu kilishuka kwa kiasi kwamba wakati Amirul Mominin (a.s.) alipouliwa kishahidi na habari zikafika Damascus (ni dhahiri kwa vile hizi hazikuwa habari za kawaida, ingawa kulikuwa na uadui lakini kila mtu alitaka kujua zaidi), mtu mmoja aliuliza: “Ali kauliwa wapi?” Mtu mmoja akajibu: “Kauliwa Msikitini.” Mtu yule mara moja akajibu kwa hasira: “Ali alikuwa anafanya nini msikitini?” Swali hili latosha kupima uadui wa mtu yule wakati alipouliza kwamba Ali alikuwa anafanya nini msikitini. Aliambiwa: “Alikuwa anaswali.” Mtu yule kwa aibu aliuliza tena: “Kwani Ali alikuwa akiswali pia?”

Sasa baada ya mafundisho na mafunzo hayo, wakati Imam Husain (a.s.) alipompinga Yazid, ilitangazwa kwamba Khariji ameasi dhidi ya Amirul Mumminin Yazid na ni wajibu kwako wewe kupigana pamoja naye (tunaomba kinga kwa Allah!). Kama Imam Husain (a.s.) angeenda bila ya familia yake (wanawake na watoto); na angekwendwa pamoja na vijana na jamaa wa kiume wa familia na wote wangeuliwa katika (ardhi

³ Surah Baqarah (2):207

ya) Karbala, ingelikuwa kitu kile kile ambacho kilikuwa kikisemwa kuanzia mwanzo, kwamba Khariji ameasi, na kulikuwa na mapigano na kila mtu aliuawa. Sasa, sababu za kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.) ambacho Allah alikitamani zingetoweka, yaani, mara tu Imam Husain (a.s.) alipopata kifo cha kishahidi, sababu kwa ajili ya kifo chake cha kishahidi vilevile zingefisha kishahidi na kungelikuwa hakuna faida yoyote ya kifo hiki cha kishahidi. Kwa hiyo, ufungwa wa familia yake ulikuwa ni muhimu kwa ajili ya kuliweka hai lengo la kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.). Hii ilikuwa ni busara ya kiungu.

Ilikuwa ni usahihi wa Allah kwamba sio tu auliwe Imam Husain (a.s.) bali na familia yake pia wawe mateka, ili kwamba popote pale wanapokwenda, walitangaze jina la Imam Husain (a.s.), lengo la Imam Husain (a.s.) na kueleza nani aliye uawa. Hivyo, sasa inakuwa wazi kwamba kwa nini Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema lazima uende kwa vile ni utashi wa Allah na usahihi kwamba lazima uuliwe na kwamba familia ichukuliwe mateka kwa sababu kuuliwa peke yako kulikuwa hakuna maana. Vivyo hivyo, Imam Hasan (a.s.) aliuliwa kwa sumu na leo waandishi wanafanya juhud kubwa kumuokoa mtawala wa Syria, Muawiyah kutokana na lawama hii. Au, wanasema kwamba haiko wazi kwamba ni nani aliyekuwa sababu kubwa ya kifo cha kishahidi cha Imam Hasan (a.s.) na watu hawalifahamu hilo. Kisha, halikadhalika ingelikuwa kabisa hivyo hivyo kwa Imam Husain (a.s.). Hii ndio maana ni kwa nini Kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.) kitakuwa sio kamili, bali kitakuwa batili, kama familia yake isingefuatana naye.

Kama watu wa familia yake wangelikuwa pamoja, basi ungeona kwamba maandalizi yote yaliyofanywa na Yazid yangerudia kwake. Unaona, kwamba anamuamuru Ibn Ziyad kuwaleta watu wa familia kutokea njia ndefu. Kwa mfano kama mtu anataka kwenda Chapra⁴ kutokea hapa, kisha huenda mpaka Bhatni⁵ kutokea hapa, kisha kutoka Bhatni mpaka Banaras⁶ na kisha Chapra⁷ kutokea hapa. Kama ambavyo kuna ukosefu wa hekima katika kuchagua njia hapo juu, kulikuwa na hekima ya dhahiri inayofanana katika kuamuru njia ndefu kwa Ibn Ziyad. Lakini Yazid hakutoa amri hii bila ya sababu. Lengo la Yazid katika hili ilikuwa (katika uhalisia hata leo njia hii kutoka Baghdad mpaka Damascus haina msongamano wa watu. Hakuna majiji na miji mikubwa katika njia hii. Watu wa mwanzo walizoea kusafiri katika njia hii kwa ngamia; hivi sasa njia hii watu wanafiri kwa magari ya abiria. Lakini hata baada ya miaka 1,400 hakuna majiji yenye msongamano wa watu katika njia hii) kiasi kwamba kama wanakuja kutoka Kufa kwenda Damascus kwa njia hii, hakuna mtu atakayekuwa kujua, wala kuwa na habari na ushindi wao mkubwa wa dhahiri. Vilevile, fahari ya na utukufu wa Yazid utakuwa haujaingizwa kwenye nyoyo za watu kwamba nguvu na uwezo ulioje aliokuwa nao huyu Yazid kiasi kwamba ameua mtu mkubwa kama Imam Husain (a.s.). Hivyo sasa kama sisi (watu) tukimpinga, hatima yetu itakuwa nini! Alitaka kuonesha nguvu zake na kuamrisha uwezo wake kwa wote. Kwa hiyo, yeye mwenyewe alichora njia ambayo ilikuwa ndio itumike. Ilikuwa njia ndefu isiyo ya kawaida ambayo ina majiji makubwa katika njia yake. Huu ulikuwa ni mpango. Lakini nini hatimaye kilichotokea?

Matokeo ilikuwa ni kwamba taarifa za kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.) ilienea katika njia kubwa. Hatimaye, takriban theluthi moja ya miji ilifunga milango yao kwa msafara huu na hawakuruhusu kichwa kitukufu cha Imam Husain (a.s.) na familia yake waingie mijini humo kama ishara ya kumkataa Yazid. Matokeo yake, badala ya hofu na woga kwa Yazid kuwashika watu, upinzani kwa Yazid ulianza kunyanya vichwa vyao. "Kamwe isijetokea kwamba adhabu ambayo ni ya kukushukia juu yenu isituzunguuke pamoja nanyi." Allah alitaka kutuonesha kwamba wanafanya mbinu na mipango yao na Mimi ninafanya mbinu na mipango Yangu. "Ewe Mtume (s.a.w.w) wape mhula na muda kwao ili kwamba waweze kufanya kazi yao. Na nitaigeuza nyuma mipango yao kwenye nyuso zao." Hivyo sasa Allah anafanya kile ambacho Yeye alikusudia. Badala ya watu kuja na hofu ya Yazid au kuvutiwa na uwezo wake, upinzani kwake ulianza sehemu nyingi.

Wakati msafara ulipowasili Damascus, tangazo lilitolewa; "Enyi watu! mtu mmoja ameasi (dhidi ya mtawala wa sasa Khalifa)."

Acha habari zote, wakiwa njiani kuelekea Syria katika soko la Damascus, mzee mmoja alielekea kwa Imam Zainul Abidin (a.s.) na akasema: "Shukuran zote ni kwa Allah kwamba ameng'oa *fitna* yenu." Imam Sajjad (a.s.) alijua kwamba mzee yule alikuwa anazungumza maneno yale kwa sababu ya kutokuelewa kwake.

4 Chapra ni takriban 65 km masthariki ya Siwan (Mtarjumi).

5 Bhatni ni takriban 60 km magharibi ya Siwan (Mtarjumi).

6 Banaras ni takriban 60 km. mashariki ya Bhatni (Mtarjumi).

7 Chapra ni takriban 60 km. magharibi ya Banaras (Mtarjumi).

Imam Zainul Abidin (a.s.) aliuliza: “Ewe mzee wangu! umesoma Qur'an?”
Yule mzee akajibu kwa kukubali.

Imam Zainul Abidin (a.s.) alimuuliza tena: “Umesoma aya hii:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسُ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُظْهِرَكُمْ تَطْهِيرًا
“Hakika si mengineyo Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu,
enyi watu wa nyumba ya Mtume, na kuwatakasa kabisa kabisa.”⁸

Yule mzee akakubali tena.

Imam Zainul Abidin (a.s.) Akafahamisha: “Ewe mzee wangu! Ahlul Bayt walijotajwa katika aya ambayo kwamba Allah ametaka kuwaondolea uchafu ni kwa ajili yetu sisi tu.”

Imam Zainul Abidin (a.s.) aliuliza tena: “Umesoma aya hii:

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةُ فِي الْقُرْبَى

“Sema: kwa haya siwaombi malipo yoyote kwenu isipokuwa mapenzi katika ndugu”⁹
Alijibu kwa kukubali.

Imam Zainul Abidin (a.s.) Akaelezea: “Sisi ni wale ndugu wa karibu ambao kwetu mapenzi yamefanywa kuwa ni wajibu.”

Imam Zainul Abidin (a.s.) Aliuliza tena: “Umesoma aya hii:

فَمَنْ حَاجَكَ فِيهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْ نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ

“Na watakao kuhoji baada kukufikia elimu hii, waambie: Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu”¹⁰
Yule mzee kwa mara nyingine akakubali.

Imam Zainul Abidin (a.s.) akatamka: “Mtoto wa Mtume (s.a.w.w.) aliyetajwa katika aya hii, ni huyu ambaye kichwa chake kimenyanyuliwa juu kwenye mkuki...”

Yule mzee akauliza huku akiwa ametatazika: “Aya hii inawahusu ninyi? Lakini sisi tumeambiwa kwamba mtu huyu ameasi! Allah amlaani mtu ambaye amemuua mtoto wa Mtume (s.a.w.w.)...”!

Hivyo, kizazi kitukufu cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), baada ya kifo cha kishahidi cha Imam Husain (a.s.) kilikuwa kinatangaza na kujulisha kuhusu kubarikiwa kwa haiba ya Imam Husain (a.s.). Kama kusudio hili halikuwa la madhumuni au lengo kubwa mbele yao, sidhani kwamba Janabe Zainab (s.a.) angekubali uso wake ufunuliwe mbele ya maelfu ya watu na kumuona. Acha mambo yote pembedi, kama khutba mbili tu – zilizotolewa na Janabe Zainab (s.a.) katika baraza la Yazid na khutba ya Imam Zainul Abidin (a.s.) katika Masjid-e-Jaame’ – zinachambuliwa lengo la ufungwa baada ya kifo cha kishahidi lingeleweka.

Sitachukua muda wenu zaidi. Unafahamu kwamba wakati mtu mmoja alipoonesha hamu yake ya kumchukua Janab-e-Fatemah Kubra (s.a.) kama kijakazi (mtumwa wa kike), alitambulishwa kwamba huyo ni Fatimah, bint wa Imam Husain (a.s.). Aliuliza: “Husain ni nani?” Alijibiwa: “Ni mtoto wa Ali na Fatimah Zahra.” Kusikia hivi, alipiga uso wake na kulia, “Niliambiwa kwamba mateka hao ni Waturuki na Wadilami... sikujua kwamba wewe, Ewe Yazid, Allah akulaani, umemuua mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kuwaleta watoto wake kama wafungwa.” Kutokana na maneno haya mazito, aliuliwa na kufa kishahidi kwa amri ya Yazid

Sasa umetambua kwamba sio tu Imam Sajjad (a.s.) na Janab Zainab (s.a.) walijitambulisha wenywewe pale Karbala bali pia tunafahamu kwamba Imam Husain (a.s.) aliuliza maswali yafuatayo:

Waulizeni masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) waliopo mionganini mwenu hivi sasa, hakuna mwingine isipokuwa mimi tu ndiye mjukuu wa Mtukufu Mtume (s.a. w.w) kwa sasa juu ya ardhi hii, mnajua kilemba hiki ni cha nani? Ngao hii ni ya nani? upanga huu ni wa nani?

⁸ Surah Ahzaab (33):33

⁹ Surah Shura (42):23

¹⁰ Surah Aale Imran (3):61

Imam Husain (a.s.) alikuwa hafanyi utambulishi huu ili apate kuhurumiwa bali kuondoa dhana potofu kutoka kwenye akili zao ili waelewe kwa ukamilifu ni nani wanamuua. Imam Husain (a.s.) alifanya hivi kukamilisha hoja juu yao. Ukamilishaji wa hoja na utangazaji pia ilikuwa ni lengo la kifo chake cha kishahidi. Kutokana na mambo haya watu wa Syria walitambua kwamba hawa ni jamaa na ndugu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), wajukuze wa kike na wa kiume.

Sasa Damascus inashuhudia hasira za watu kwa kiasi kwamba Yazid alilazimika kufikiria kuhusu kuikabali hali hiyo.

Aliamuru watu wote kukusanyika saa moja kabla ya swala ya Dhuhr na kumpa amri khatibu (mzungumzaji wake), ambaye alikuwa ni msaidizi wake, kumpaka matope Amirul Muminin Ali (a.s). na Imam Hasan (a.s.) kwa kiwango cha juu iwezekanavyo na kumsifia Yazid. Lau asingemtaka Imam Sajjad (a.s.) kuhudhuria mkusanyiko huo, lengo lake kubwa pia lingekamilika. Lakini Allah aliuvunja mpango wake huu mikononi mwake kabisa palepale. Alifikiria Imam Sajjad (a.s.) atasikiliza tu alichokua akisema kwa muda wa saa nzima huku akiwa amenyamaza bila ya kupinga. Imam Sajjad (a.s.) alikuwa amefungwa minyororo na pingu na kukalishwa karibu na mimbari. Khatibu akaongea kile ambacho alitaka kuongea na Imam Sajjad (a.s.) kwa subra alivumilia. Hatuwezi kutambua ni maumivu ya kiasi gani alihisi Imam Sajjad (a.s.).

Wakati Khatibu yule aliponyamaza, Imam Sajjad (a.s.) alimuambia (yule khatibu) kwamba amepata hasara kubwa kwa ajili ya Yazid. Umemchukiza Allah ili kumpendeza Yazid na umejihakikishia makazi yako katika Jahannamu.

Yeye (a.s) kisha alimuomba Yazid kwamba alitaka kupanda juu ya mimbari na kusema kile ambacho kitakuwa na manufaa kwa watu.

Yazid alikuwa anafahamu matokeo ya kumruhusu Imam Sajjad (a.s.) kupanda juu ya mimbari na hivyo alikuwa akifanya visingizio tofauti. Lakini kutokana na msisitizo wa watu, mwishowe alikubali na kumruhusu Imam Sajjad (a.s.) kuzungumza juu ya mimbari.

Mrithi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikaa juu ya mimbari katika hali ambayo si Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wala Imam Ali (a.s.) alikaa juu ya mimbari kama hivi kabla. Alikaa kwenye mimbari bila ya kilemba kichwani mwake, wala joho sahihi mwilini mwake; nguo zake zilikuwa zimechanika chanika, minyororo shingoni mwake na mikono na miguu yake ikiwa imefungwa. Baada ya kumshukuru Allah, yeye (a.s.), alianza khutba yake: "Shukran kwa Allah katika neema halikadhalika katika shida; shukran kwa Allah kwamba Yeye ametutunuku sisi hadhi sita (za ubora) na sifa njema saba. Ametupatia sisi ilmu, uvumilivu, ukarimu, utukufu, ari na ameingiza mapenzi yetu katika nyoyo za watu. Ama kwa sifa njema, Mtume Muhammad (s.a.w.w.), muaminifu mkubwa Ali Ibn Abi Talib (a.s.), Janab Jafar al-Tayyaar (a.s.), simba wa Allah na simba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.a.), Janab Hamza (a.s.) na mabwana wa vijana wa Peponi, Imam Hasan (a.s.) na Imam Husain (a.s.) wanatokana na sisi.

"Enyi watu! Wale ambao wananjua mimi, wananjua, na wale ambao hawanijui mimi, najitambulisha mwenyewe kwenu kuititia nasaba na jadi yangu. Mimi ni mtoto wa Makka na Mina, ni mtoto wa Zamzam na Safa."

Aliendelea kujitambulisha mwenyewe mpaka aliposema: "Mimi ni mtoto wa yule ambaye Allah alimchukwa kutoka Makka mpaka Baitul Maqdas, kisha akapandiswa mpaka mbinguni, kwenye Arsh Yake, mpaka kwenye Sidrah al-Muntaha, mpaka yeye (s.a.w.w) akaja mpaka Kwake kwa umbali wa kamba ya uta mpaka kati ya uta. Mimi ni mtoto wa yule ambaye alikula kiapo mara mbili kwenye mikono ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), ambaye alipigana kwa panga mbili, ambaye alipigana kwa mikuki miwili, ambaye alihama mara mbili, na hakuna anayelingana naye katika nasaba, shujaa na mpole, ambaye kwa upanga wake Uislamu ulisimama na kwake yeye misingi ya Uislamu ikawa imara; kama humjui, basi elewa kwamba yeye ni Ali ibn Abi Talib (a.s.)."

Sasa, kile kilichosemwa mwanzo kilikuwa kinafutwa. Baada ya kuelezea kwa kina ubora wa Amirul Muminin (a.s.), aliendelea kusema: "Mimi ni mtoto wa yule ambaye kwake aya ya 'HAL ATAA' iliteremshwa". Baada ya kusimulia mambo yote haya, yeye (a.s) alisema: "Eleweni kwamba yeye ni Ali Ibn Abi Talib (a.s.)".

Baada ya hapo, ye ye (a.s) alianza kumtambulisha Janab-e-Zahra (s.a.): "Mimi ni mtoto wa Mtume wa Mwisho (s.a.w.w.), mimi ni mtoto wa Bibi wa mabibi wa walimwengu." Mwishowe, alifika kwa Imam Husain (a.s)... "Mimi ni mtoto wa mtu yule ambaye mumemuita kama mgeni lakini hamkumkaribisha. Mimi ni mtoto wa mtu yule ambaye shingo yake ilikatwa kwa nyuma yake. Mimi ni mtoto wa yule ambaye mwili wake ulipondwa pondwa na farasi. Mimi ni mtoto wa yule ambaye kichwa chake kimenyanyuliwa juu ya mkuki. Mimi ni mtoto wa mtu yule ambaye mwili wake uliharibiwa. Mimi ni mtoto wa mtu yule ambaye mahema yake yalichomwa moto. Mimi ni mtoto wa mtu yule ambaye mabega ya wanawake wa familia yake yalifungwa kwa kamba. Mimi ni mtoto wa mtu yule ambaye familia yake ilichukuliwa mpaka kwenye miji na majiji. Mimi ni mtoto wa yule mtu ambaye mwili wake ulilala siku tatu bila kufunikwa nguo."

Athari ya khutba hii ilikuwa yenyenye nguvu mnno sana kiasi kwamba kila mtu Msikitini mle alianza kulia kwa sauti kubwa na watu waliokuwa wamekaa karibu na kuta walikuwa wanapiga vichwa vyao kwenye kuta hizo.

Yazid, ambaye alikuwa akishuhudia mandhari hii kwa umakini, alitambua kwamba kama Imam Zainul Abidin (a.s.) ataendelea na khutba yake, kutakuwepo na mapinduzi. Wakati huo huo, Yazid hakuweza kumnyamazisha Imam Zainul Abidin (a.s.) na kumfanya ashuke kutoka kwenye mimbari. Kwa hiyo, alimuamuru "Muadhini" aadhini, akijua kwamba hili moja kwa moja litakata mara moja khutba ya Imam Zainul Abidin (a.s.). Lakini alikosea kupima ushujaa na akili ya Imam (a.s.). Imam Zainul Abidin (a.s.) alisimamisha khutba yake lakini hakushuka kwenye mimbari. Wakati Muadhini aliposema: "Allah ni Mkubwa", Imam Zainul Abidin (a.s.) akashuhudia kwamba Allah ni Mkubwa. Muadhini alipofikia kusema: "Nashudia kwamba Muhammad (s.a.w.w.) ni Mjumbe wa Allah", Imam Zainul Abidin (a.s.) alimsimamisha Muadhini kuendelea na Adhana, kisha akamgeukia Yazid na aauliza: "Niambie, Ewe Yazid, Muhammad (s.a.w.w) ni babu yako au babu yangu mimi? Kama ukisema ni babu yako, utakuwa ni uwongo wa dhahiri na kama ukisema ni babu yangu, basi kwa nini umemuua mtoto wake na kuwafunga?"

Yazid alikuwa kimya na akaondoka msikitini pale kwa aibu.

Hii ndio maana Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema kwamba Allah anapenda kwamba unauliwa kishahidi, wanawake wako na watoto watakuwa wafungwa ili kwamba watu waelewe lengo lako kubwa na kuitambua familia yako. Lengo hili lilikamilishwa katika hali ambayo Yazid hakuwa na hiyari bali kuwaachia wafungwa wale.

Yazid alimuita Imam Zainul Aabidin (a.s.) na akasema: "Nataka kukuacha huru sasa. Ni matakwa yako, kama unataka unaweza kwenda Madina au endelea kuishi nasi kwa heshima na amani" Imam Zainul Aabidin (a.s.) akajibu: "Ngoja nishauriane na shangazi yangu (Zainab) na kisha nitarudi kwako." Zainab (s.a.) akajibu kwamba: "Tutarudi Madina lakini muambie Yazid kwamba sijamlilia kaka yangu tangu auliwe kishahidi. Hivyo, tuachini baraza ili tuweze kuwaombeleza mashahidi wetu." Maombolezo, kulia na kupiga vifua kuliendelea kwa muda wa siku nane katika kasri (ikulu) ya Yazid.

Yazid (l.a.) alimuita Noman bin Bashir, ambaye alikuwa akijiita sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akamtaka afanye maandalizi ya safari yao. Maelezo haya yanauhuzunisha moyo sana. Matandiko ya hariri (ya farasi) yaliandaliwa pamoja na mapazia ya hariri; na kikosi cha kuhakikisha usalama wao kiliteuliwa ili kwamba wakati wanawake wakisafiri watembee mbele yao na wakati wakisimama, waweke kambi mbali na Ahlul Bayt (a.s) ili kwamba wasiweze kuwaona.

Ningependa kumuuliza Yazid (l.a.) kwamba hawa ni zile zile nguzo zenye kuongoza za umaasum ambao shingo zao na mikono ilikuwa imefungwa. Imam Zainul Aabidin (a.s.) anasema kwamba shingo kumi na mbili zilifungwa kwa kamba moja na waliburuzwa katika masoko kama kundi la kondoo. Leo, maandalizi mengi yanafanywa kwa ajili yao. Hata hivyo, mabibi wale walipitia Karbla kabla ya kuwasili Madina.

Msafara huu sasa unawasli Madina kutoka Syria. Kuanzia wakati wa Hashim (a.s.), kwa kweli hata kabla ya hapo, misafara ambayo ilikuja kutoka Syria ilikuwa ikisimama kwenye sehemu iliyotengwa na kupiga kambi hapo. Hivyo, kuna sehemu mpaka leo nje ya viunga vya Madina ambayo inaitwa Shamia, yaani, misafara ambayo inatokea Syria (Sham) husimama hapa. Wanaweka mahema yao hapo bidhaa zao na kutembelea mjini Madina kila siku kwa ajili ya kuuza bidhaa zao na kurudi hapo. Hata leo ni hivyo hivyo. Watu wa

mwanzo walikuja kwa ngamia, leo wanakuja kwa magari ya abiria. Magari ya abiria yanayotoka Syria husimama Shamiya. Ni kama kituo chao cha magari yao ya abiria.

Nilitembelea sehemu hiyo wakati huu. Kwa vile kulikuwa na sharti katika Hajj kwamba mtu hawezi kusafiri ndani ya gari lililofunikwa, hivyo tulitafuta gari la wazi, mtu mmoja akutuelekeza Shamiya kwa matumaini kwamba tunaweza kupata gari la wazi huko. Kwa njia hii, nilizuru Shamiya. Hatukupata gari tulilotlaka pale, lakini huzuni kubwa ilitushika kujuu kwamba hii ni sehemu ile ile ambako Imam Sajjad (a.s.) aliwasili na kuamuru kuweka kambi ya mahema yake hapo na kisha akamuuta Bashir Ibn Juzlam na akasema: "Ewe Bashir! Allah amrehemu baba yako! Alikuwa msahairi. Je, wewe wasoma mashairi?" Akajibu kwa kuitikia. Imam (a.s.) akamuamuru: "Basi henda na uifahamishe Madina kuwasili kwetu." Bashir alimpanda farasi wake na akaondoka kuelekea mjini Madina. Alikuwa kimya mpaka alipowasili Masjid-e-Nabavi (s.a.w.w.). Alipowasili hapo, alipiga ukulele:

*Enyi watu Madina! Haifai ninyi kuishi mjini hapa,
Husain aliuliwa kishahidi katika mchanga wenye joto na macho yanya yanalia
Ilikuwa sharti kwamba mwili wa Husain ulikuwa umelala katika mchanga wenye joto ukiwa umepakazwa damu
Na kichwa chake kilinyanyuliwa kwenye mkuki na kilichukuliwa kutoka mji mmoja hadi mwengine.*

Mara tu waliposikia ukelele ule, wazee na vijana kwa pamoja walitoka nje ya nyumba zao mara moja. Bashir alitangaza kwamba Imam Zainul Aabidin (a.s.) amekuja pamoja na Ahlul Bayt (a.s.) na ameshukia Shamiya. Wote walikimbia kuelekea sehemu hiyo. Wanawake walikuwa wanapiga nyuso zao, baadhi walikuwa wanapiga vifua vyao na kulikwa na vilio na maombolezi kiasi kwamba wachunguzi wanasema kwamba maombolezi hayo yalikuwa kama yale ya wakati wa kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wakati Bashir aliporudi, hakupata njia ya kumfikia Imam Sajjad (a.s.). Kulikuwa na msongamano mkubwa wa watu na kwamba alisema alimuacha farasi wake na kumfikia Imam Sajjad (a.s.) kwa kukanyaga juu ya mabega ya watu. Wakati nilipowasili, nilimuona Imam Sajjad (a.s.) akitoka nje ya hema lake. Mmoja wa watumishi alimletea kiti na Imam Sajjad (a.s.) akakaa. Imam Sajjad (a.s.) alikuwa amevaa kitambaa cheusi mkononi mwake. Alikuwa analia.

Hebu tufikirie kwamba kama tulikuwa kwenye safari na kama watoto wetu au ndugu zetu wakafariki, wakati wa kurudi tutanyamaza mpaka Siwan. Tutakuwa kimya njiani kote wakati wa kurudi lakini wakati tukiwaona jamaa zetu na marafiki zetu, tutaangua vilio na kulia kwa sauti. Hii ilikuwa ndio hali ya Ahlul Bayt (a.s.) na Imam Zainul Aabidin (a.s.). Wakati alipopata utulivu, Imam Sajjad (a.s.) alianza kusimulia matukio na mwishowe alisema: "Enyi watu wa Madina! Kama babu yangu angewaambia ummah wake kuwakandamiza Ahlul Bayt (a.s.) kwa kiasi inavyowezekana, wauwe na kuwakata vichwa, ummah usingetukandamiza zaidi kama ambavyo wamefanya licha ya yeye (s.a.w.w) kuacha wosia kwa ajili ya mapenzi kwetu."

Sasa, kwa amri ya Imam Sajjad (a.s.), msafara ukaondoka kuelekea mjini Madina. Baada ya kuingia mjini, kwani walifika kwenye Msikiti wa Mtume (s.a.w.w). Wakati walipoingia Mjini wa Madina, Janabe Umm Kulthum (s.a.) hakuweza kuvumilia (kukaa kimya kwa huzuni), alilia kwa sauti kubwa na akaanza kusoma ubeti ufuatao:

*Ewe mji wa babu yangu, usitukaribishe.
Kwa vile tunakuja na masikitiko na huzuni.*

Aliendelea:

*Ewe Madinah! Wakati tunaondoka na kukuacha tulikuwa na familia kamili.
Lakini sasa wakati tunarudi, hatuna walezi na maula wetuwala hatuna watoto wetuwetu mikononi mwetu;
tumewapoteza wote.*

Wakati alipotupa jicho upande wa Jannatul Baqi, alilia kwa sauti huku akisema:

*Ewe (mama) Fatima! Natamani ungetuona jinsi ambavyo tulifanywa wafungwa na kuzungushwa kutoka mji
mmoja hadi mji mwengine na kitongoji hadi kitongoji.*

Janabe Zainab (s.a.) alikuwa mgonjwa mpaka sasa lakini wakati alipofika kwenye Kaburi la babu yake, alikamata mnyororo na kusoma sentensi mmoja:

Ewe babu yangu! nimekuja pamoja habari za huzuni za kifo cha mjukuu wako Husein (a.s.).